**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI -SONGWE**

**Shule ya Sekondari Msia,**
**S. L. P 522,**
**MBOZI.**
**Tarehe…………………..**

**Namba za simu;**
**Mkuu wa Shule: 0754 - 514079**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0767 - 767442**
**Patron: 0742 - 027125 / 0757 - 108901**

**Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi**
**.....................................................................................**
**S. L. P .....................................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSIA…………….**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka **………………………………………** na atasoma tahasusi ya ..........................................................

Shule hii ipo katika Wilaya ya ***Mbozi,*** Mkoa wa ***Songwe***, ipo kilometa **28** kutoka mji mdogo wa ***Mlowo*** barabara kuu ya ***Mbeya - Tunduma***. Kama unatokea njia ya Iringa unapanda gari linaloishia Mbeya, teremka stendi ya ***Nanenane*** au stendi kuu ya mabasi jijini Mbeya, Kisha panda daladala kuelekea stendi ya mabasi madogo iliyopo Uwanja wa ndege wa zamani, maarufu kama ***(Airport ya zamani)*** kwa nauli ya shilingi 1,000/= Kisha panda magari ya kwenda Tunduma ***(Coaster)*** halafu shuka Kituo kiitwacho ***Stendi mpya (Mlowo)*** kwa nauli ya shilingi ***4,000/=*** Baada ya hapo panda magari yaendayo Msangano kwa nauli ya shilingi 7,000/= au pikipiki kwa nauli ya shilingi ***10,000/=*** na ushuke kijiji cha ***Msia*** eneo liitwalo Iyunga. Aidha akama unatokea Njia ya Sumbawanga shuka eneo hilohilo la ***Stendi Mpya (Mlowo)*** na ufuate maelekezo ya usafiri kama hapo juu.

Aidha kwa atakayepanda usafiri unaoenda moja kwa moja hadi Tunduma, huna haja ya kushuka Mbeya, shuka moja kwa moja ***Stendi Mpya (Mlowo)***, kisha fuata maelekezo ya hapo juu.

Muhula wa masomo utaanza tarehe……………**…**hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe **…………………………………...**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

Sare ya Shule hii ni kama ifuatavyo;

(i) Suruali mbili, Moja rangi ya kijivu na ya pili ni rangi ya khaki

(ii) Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu (imara na nadhifu)
(iii) Jezi (bukta na fulana) rangi ya *blue (Chelsea blue) pamoja* na viatu vya michezo (iv) Viatu vya Shule *vyeusi* vya ngozi, vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (v) Soksi jozi mbili nyeusi za Shule
(vi) Mkanda *mweusi* wa ngozi wa kuvalia suruali usio na chuma kubwa wala picha wala alama za hatari (mfano: alama ya fuvu)
(vii) Sweta rangi ya *zambarau,* (endapo utalikosa linapatikana shuleni)
(viii) Nguo za kushindia *(shamba dress)* ni suruali mbili rangi *ya "dark blue"* na "T - shirt" ya *kijivu.* (Endapo utaikosa inapatikana shuleni)
(ix) "T - shirt" Moja yenye kola (form six) rangi ya *"dark blue"* (endapo utaikosa inapatikana shuleni)
(x) "Track suit" nyeusi isiyo na maandishi
(xi) Kandambili kwa ajili ya kuogea tu

2.2 MAHITAJI MENGINE
(i) Madaftari 10 (Counter books - *Ouire 4)*
(ii) "Ream (A4)" za karatasi mbili (2) aina ya "Rotatrim"
(iii) Vitabu vya Masomo ya Tahasusi husika. (Orodha imeambatishwa)
(iv) "Scientific calculator" 01 (Kwa wanaosoma HGE)
(v) Godoro imara *la futi 2.5 kwa futi 6*
(vi) Shuka 02 rangi ya pink, Blanketi 01, chandarua 01 rangi ya *"blue"*
(vii) Nguo za ndani za kutosha
(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
(viii) Ndoo 02 ndogo *(lita 10)* zenye mifuniko
(ix) Kwanja 01, jembe 01, reki 01 na mifagio 02 (wa ndani na nje)
(x) Tochi 01 kwa ajili ya dharula mwanga unapokosekana

2.3 MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MICHANGO | KIA SI |
|---|---|---|
| 01 | Mchango wa uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 02 | Tahadhari | 5,000/= |
| 03 | Nembo ya shule | 5,000/= |
| 04 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | JUMLAKUU | 80,000/= |

Kumbuka: Fedha za michango tajwa hapo juu zilipwe kupitia akaunti ya Shule; yenye jina; *MSIA SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION, AKAUNTI NAMBA: 61202000010 NMB.* (Tafadhali fika na *"pay in slip"* yenye jina la Mwanafunzi husika)
N.B Kila Mwanafunzi anatakiwa kuchangia shilingi 50,400 *kwa* ajili ya Bima ya Afya. Ikiwa anayo Bima ya Afya aje na kitambulisho cha Bima ya Afya

3. (a) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya sekondari Msia inaendeshwa kwa mujibu wa *sheria ya Elimu Na.25* ya mwaka *1978.* Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia sheria na miongozo ifuatazo uwapo shuleni, ambazo zitafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, Wazazi na Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine najamii kwa
b) ujumla ni jambo la lazima(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
c) Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku *(Evening Reparation)*
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo
f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za shule
j) Ni marufuku Mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, wala taarifa ya Mwalimu au Patron
k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi Mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

(b) MAAGIZO MENGINE MUHIMU

1. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna Mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya Mwanafunzi.
2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku Mwanafunzi kuala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa.
3. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
4. Mwanafunzi anapaswa kutambua malengo yaliyomleta shuleni na hivyo anapaswa awe na NIDHAMU ya hali ya juu iii kukabili vyema masomo yake na kutimiza ndoto zake; Uongozi wa shule hautasita kumrejesha nyumbani mwanafunzi yeyote asiyefuata ratiba, sheria na taratibu za shule.
5. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au ugonjwa)

Kumbuka: Kwa kuwa Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu / laini, Shule imeweka utaratibu kwa Wazazi/Walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu namba *0768626199* (Jina: *Hashbon Kanyika -Muhasibu wa Shule)*

(c) MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria rnasorno kwa zaidi ya *siku 90* bila taarifa / utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au kupigana kwa namna yoyote ile.
vi. Kufuga ndevu au nywele
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uasherati, uhusiano wajinsi moja, kuoa au kuolewa
ix. Kusababisha ujauzito au kutoa mimba Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
x. Kuingia kwenye majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xi. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xii. Kudharau Bendera ya Taifa
xiii. Kufanyajaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xiv. Uharibifu wa mali yoyote ya shule rra ya umma kwa makusudi
xv. Kulala au kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa ya *MKUU WA SHULE.*

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

Fomu ya Uchunguzi wa Afya *(Medical Examination Form)* ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa yajinai.

i. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

ii. Picha tatu (3) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

*Kumbuka:* Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na wimbi la utepeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni Mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi, hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE ,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWEI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:

Mkuu wa Shule: 0754 – 514079, Makamu Mkuu wa Shule: 0620-241539

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MSIA

PATRICK TALEON MZENA

MKUU WA SHULE

...IYA SEKONDARI

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MSIA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 522,
MBOZI.
DATE ............................

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL ..............
P.O.BOX .......................................

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine ........................................................................(student name) as to his fitness for pursuing further Education at this school.

.......................................
**HEADMASTER**

1. Haemoglobin ............................................................................
2. P.V. Bleeding ..........................................................................
3. Blood Pressure (BP).....................................................................................
4. Blood Group ...........................................................................
5. (a) Sight ................................................................................
   (b) Hearing ............................................................................
6. Urine for sugar ....................................................
7. Stool for routine–Examination ..........................................................
8. Asthma ..................................................................................
9. Skin diseases ...........................................................................
10. Epilepsy ...............................................................................
11. Leprosy ................................................................................
12. Pulmonary Tuberculosis ..............................................................
13. Deformity ..............................................................................
14. Mental problems .......................................................................
15. V.D. (Give type) ......................................................................
16. Any other serious disease not mentioned above.......................................

OTHER COMMENTS .............................................................

DESIGNATION AND SIGNATURE

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI MLANGALI**
**FOMU YA AHADI MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI:

(a) Mimi ………………………………..nimezaliwa tarehe ………...................... Jina la Baba .............................................. Jina la Mama …………………….............. Aujina la mlezi ……………………………. nakubali kuingia kidato cha ………... katika shule ya Sekondari MSIA kama mwanafunzi wa bweni. Nitafika shuleni tarehe ………………… bila kukosa au kuchelewa.

(b) Nitatii sheria zote za shule kama zinavyosomeka na nitaishi maisha mazuri ya mfano hapa shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea. Sitakuwa mtoro shuleni. Wala kuwa mwanafunzi mwenye usumbufu wa aina yoyote ile . Naahidi kutoshiriki migomo ya aina yoyote ile hapa shuleni.

(c) Saini ya mwanafunzi……………………….................. Tarehe ……….........................

## B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:

1. Mimi ……………………………….. ninakubali mtoto wangu Gina) ………………… Asome katika shule ya Sekondari Mlangali kuanzia tarehe……………………………….
   Ninaamini kuwa Elimu ni urithi wa mtoto na **MWANGA WA MAISHA YAKE**
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ulivyoagiza katika barua yako. Nitatoa na kutekeleza kwa wakati na bila usumbufu wowote.
3. ninaahidi kulipa michango ya shule kwa wakati inapohitajika. Vinginevyo nichukuliwe hatua kali, mimi Mzazi / Mlezi.
4. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na ya mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asiwe mtoro na msumbufu.
5. Ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya Sekondari Msia kama mwanafunzi wa bweni ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha sita
   (1) Mimi sitamhamisha kwenda shule nyingine pasipo sababu.
6. Anuani yangu ya kudumu ni.-
7. Namba ya simu :…………………………………………….
8. Sahihi : …………………………………….

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU:**

Mwanafunzi ……………………………………………………………………amepokelewa tarehe : …………………………………………………………… anamapungufu ya vifaa vifuatavyo:
1………………………………………….. 2. ……………………………………………………..
3………………………………………… 4. …………………………………………………….

**SAINI: ……………………………………………**

MWALIMU ANAYEPOKEA

TAARIFA BINAFSI

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika kidato cha nne .
   Dini / dhehebu

2. Jina kamili la baba Mzazi / Mlezi ........
   Kazi yake ......
   Anwani kamili ya baba mzazi /mlezi ..........................................................

   Namba ya simu ya mkononi

   Mahali anakoishi baba mzazi / mlezi. Mkoa Wilaya .

   Tarafa Kijiji / Mtaa .

   Jina kamili la Mama mzazi / Mlezi .
   Kazi yake .

   Anwani kamili ya mama mzazi /mlezi ........................ .................... .

   Namba yake ya simu ya mkononi .... ......................................

   Mahali anakoishi mama / mlezi: Mkoa .......................... Wilaya .... .

   Tarafa Kijiji / mtaa .

3. Taarifa ya ndugu wa karibu wanaoweza kushirikishwa kwenye malezi ya mwanafunzi awapo hapa shuleni. ..........................................................

mwana unzi awapo apa s u eni.

| JINA KAMILI | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI | ANWANI NA NAMBA YAKE YA SIMU | PICHA YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 1. (BABA MZAZI) | | | | |
| 2.(MAMA MZAZI) | | | | |
| ] . (MLEZI) | | | | |

**BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI**

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingan a na masomo yake kwa kufuata mchanganuo ufuatao

| | |
|---|---|
| **HISTORY**<br>1. Advanced Learners World History by Idrisa Msuya book 1 & 2<br>2. Essentials of Advanced Level History paper 1 & 2 by Saleh Yasin<br>3. Advanced Level History 1 & 2 by K. Shibitali<br>4. Medieval Ages paper 2 by Mavunde<br>5. A History of Africa VOL.I & VOL.II by Assa Okoth | **BASIC APPLIED MATHEMATICS**<br>1. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools Form V by Septine I. Sillem 2014<br>2. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary School Form VI by Septine I. Sillem 2014<br>3. Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Form V & VI by TIE |
| **ECONOMICS**<br>1. Economics 1 &2 by Tayebwa Mugisha<br>2. Modern Economics Theory by Dewelt<br>3. Essential Economics 1&2 by Odhiambo<br>4. Modern Economics 20th Edition by Ahuja | **GEOGRAPHY**<br>1. Integrated Approach in Geography by David Waugh<br>2. A Comprehensive Approach in Physical Geiography by D. T Msabila (2018)<br>3. Physical Geography by Zisti Kamili 2nd Edition 2016<br>4. Comprehensive Physical Geography for Secondary School by O. Mpalaki & F. Lighuda |
| **ENGLISH LANGUAGE**<br>Oxford Advanced Learners Dictionary | **KISWAHILI**<br>Kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili (Oxford) |